# Kigamboni 2021

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni Julai-Septemba 2021 Toleo Namba 01

JARIDA LA MKUSANYIKO WA HABARI MBALIMBALI

## Manispaa ya Kigamboni kinara wa 2 ukusanyaji mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021,Miradi kababmbe yatekelezwa kwa mapato ya ndani.



*Mmoja wa mradi wa uliotekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kwa kujenga nyumba ya Mkurugenzi karibu na eneo la ofisi ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa wakati.*

## YALIYOMO

DC Fatma alivyowaondoa hofu wananchi chanjo ya Uviko 19



Baraza la Madiwani laiomba Wizara ya Ardhi kuachia eneo la Tungi dampo





*Watendaji wa Kata wakiwa wameketi kwenye pikipiki zao mara baada ya kukabidhiwa.*



*Mwalo wa Samaki*

# KIGAMBONI 2021

## TAHARIRI

Karibuni wapenzi wasomaji wa Jarida letu la Kigamboni 2021 lililosheheni taarifa mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matukio yaliyofanyika kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022. Jarida hili litakuwa likitolewa mara nne katika mwaka  wa Fedha yaani kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhabarisha umma kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Manispaa.

## UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ni moja kati ya Manispaa 5 zinazaounda Jiji la Dar es  Salaam ambapo upande wa Kusini mwa Jiji hilo inapakana na Wilaya ya Mkuranga na Mashariki inapakana na Bahari ya Hindi (fukwe yenye urefu wa Kilomita 60).

Awali Kigamboni ilikua sehemu ya Manispaa ya Temeke mpaka mwaka 2015 ilipotangazwa rasmi kupitia gazeti la Serikali lenye GN No.462 kuwa Manispaa Kamili inayojitegemea. Hata hivyo Kigamboni  ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake kama Manispaa Mnamo Septemba 2016.

Kijiografia Kigamboni ina ukubwa wa Kilometa za mraba 577.9 sawa na Hekta 57.786.8 ambapo kiutawala Kigamboni ina Tarafa 3 yaani Kigamboni, Somangila na Pembamnazi, Kata 9 na Mitaa 67. pia ina jumla ya Madiwani 13 kati yao Diwani mmoja ni Mbunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Idadi ya Watu wa kigamboni inakadiriwa kuongezeka kutoka sensa ya mwaka 2012 iliyokuwa na jumla ya watu 162,932 (wanawake 51.9% wanaume 49.1% mpaka kufikia watu 225,938 (wanaume 44.6% wanawake 55.4% mwaka 2018. Idadi kubwa ya watu wa Kigamboni ni Vijana kunzia miaka 20-34 , pia wapo watoto wengi wenye umri chini ya miaka 5 ambapo idadi ya wazee wenye umri kuanzia 60 ni ndogo ukilinganisha  na makundi mengine.

Eneo kubwa la Kigamboni ni tambarare lenye muinuko kati ya 20m-50m, ina maeneo machache yaliyoinuka zaidi ya 100m-120m, ambapo eneo kubwa bado halijaendelezwa mbali na kuwa limekwishapimwa kwa asilimia 60.

Shughuli kuu za kiuchumi ambazo wananchi wake wanategemea ni Kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara na utalii.

**DIRA(VISION)**

Kuwa na jamii iliyoelimika na yenye maisha bora kufikia  2025

**DHAMIRA( MISSION)**

Kutoa huduma bora za kijamiii na kiuchumi kwa kutumia kiufasaha rasilimali zilizopo na utawala bora kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi

# KIGAMBONI 2021

## BODI YA WAHARIRI

ERASTO N. KIWALE - MKURUGENZI MANISPAA YA KIGAMBONI

## MWANDISHI

ALDA PHESTOR SADANGO

## WAHARIRI

EDWIN OWAWA- MKUU WA KITENGO CHA TEHAMA

HAPPY MKIARU- AFISA TEHAMA

PRAYGOD MNDEME- AFISA TEHAMA

ISSA MSANGI-AFISA TEHAMA

JOSEPH SEMKIWA-AFISA HABARI

ELIAS MAFWELE-MCHUMI

## LINATOLEWA NA:

Kitengo cha Teknolojia Habari na Mawasiliano
Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni
S.L.P 36009
Dar es Salaam
**Email:**info@kigambonimc.go.tz **Tovuti:** www.kigambonimc.go.tz

Kigambonimanispaa

# KIGAMBONI 2021

## Miradi kabambe iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani

Kama tunavyofahamu, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwamba ilikua sehemu ya Manispaa ya Temeke hadi hapo tangazo la Serikali mwaka 2015 kwa GN No. 462 lilipotangaza rasmi kuwa Manispaa inayojitegemea na kuanza majukumu yake rasmi Septemba 2016.

Tangu kuanzishwa kwa Manispaa hii ya Kigamboni kwa upande wa suala la usimamizi na ukusanyaji mapato imekua ikifanya vizuri, kwani uongozi wa Manispaa ulijipanga vizuri kuhakikisha malengo waliyoweka yanafikiwa hususani ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kihistoria Manispaa ya Kigamboni kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilianza na kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 2.8 ambapo hali ya makusanyo iliendelea kuwa nzuri hadi kufikia kukusanya Bilioni 8.1. kwa mwaka wa fedha 2020/2021 .

Aidha kwa kipindi chote cha miaka minne Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboi imekuwa ikipata Hati safi.

Mnamo Agosti mwaka huu Waziri wa TAMISEMI Mhe. Ummy Mwalimu alitangaza Manispaa zilizofanya vizuri kwenye ukusanyaji mapato na kuiainisha Kigamboni kuwa Manispaa ya 2 kwa Manispaa zote Tanzania.

**JITIHADA ZILIZOFANIKISHA UKUSANYAJI MZURI WA MAPATO.**

Mhasibu wa Mapato wa Manispaa Chrisostom Malingumu alisema kwanza timu ya mapato ilifanikiwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kulipa ushuru na kodi hivyo imesaidia wananchi kulipia tozo na ushuru bila shuruti

Alisema pia kwa vyanzo vya mapato vilivyopo, Manispaa iliweza kuandaa vikosi kazi vya ufuatiliaji kwa kila chanzo na vilitakiwa kuwasilisha taarifa kwenye vikao vya Menejimenti hali iliyopelekea uwajibikaji kuongezeka kwani suala la mapato liliwekwa kuwa la kila mtumishi na kila Idara.

Aidha aliongeza kwa kusema kuwa Manispaa ilifanikiwa kukusanya mapato vizuri kwa kutoa motisha kwa vikosi kazi vinavyofanya kazi ya ufuatiliaji mapato hali iliyopelekea kufikia malengo.

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO**

Katika kutekeleza Agizo la Serikali la kuhakikisha fedha za mapato ya ndani zinatumika kutekeleza na kukamilisha miradi kwa asilimia 100 ili wananchi waweze kuona faida za mapato ya ndani na hatimaye kuongeza mwamko wa ulipaji kodi na ushuru, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilifanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo kwa kutumia mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2021:

### UJENZI WA SHULE YA MSINGI MPYA YA KISASA YA GEZAULOLE.

Mradi huu ulianzishwa ikiwa ni mbadala wa shule ya sasa ya msingi Gezaulole iliyopo pembezoni mwa bahari ya Hindi. Mipango ya baadae ya Halmashauri ni kuivunja shule ya awali ili kupisha shughuli za uwekezaji wa ujenzi wa Bandari na Soko la Samaki kama mradi mkakati wa kuongezea mapato Halmashauri.

Aidha Shule ya zamani inamazingira hatarishi kwa wanafunzi hasa muda wa mafunzo kufanya baadhi ya wanafunzi ambao sio waadilifu kutumia muda mwingi kukaa baharini kuliko kusoma.

Ili kufanikisha hili Halmashauri ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo inatekeleza mradi wa ujenzi wa Shule mpya ya Gezaulole yenye jumla ya madarasa kumi na mbiili (12) na ofisi tatu (3) za walimu, ujenzi wa choo chenye jumla ya matundu kumi na mbili (12) ambayo yanatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Katika ujenzi wa Shule hii Halmashauri ya Manispaa ilifanikiwa kuchangia Milioni 75, Mfuko wa Jimbo Milioni 32, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Milioni 10.5 na CRDB Bank Milioni 30.



*Ujenzi wa Shule ya Msingi mpya Gezaulole*

# Miradi kabambe iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani

**KITUO CHA AFYA KIMBIJI-UJENZI WA JENGO LA XRAY**

Kituo cha afya kimbiji ni miongoni mwa vituo vya afya nchini vilivyopandishwa hadhi kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo Manispaa ya Kigamboni ilitenga kiasi cha Milioni 80 kujenga jengo la X-Ray kwa lengo la kuboresha utoaji huduma za kiuchunguzi kwa njia ya mionzi.

Ujenzi huu ulikuwa wa miezi 3 kuaniza 22/02/-22/05 2021 kwa kutumia force account ambapo hadi kufikia sasa mradi upo asilimia 90 ya utekelezaji na jumla ya Milioni.60 zimekwishatumika na sasa imebaki hatua ya uingizaji wa X-Ray mashine.

Kukamilika kwa mradi huu kunatarajiwa kuhudumia jumla ya wagonjwa 360 kwa mwezi hali itakayopelekea kuongeza upatikanaji wa huduma za kiuchunguzi kwa njia ya mionzi na hii itapunguza rufaa za wagonjwa, pamoja na gharama kwa wahitaji wa huduma hiyo na kuongeza mapato ya kituo.




*Jengo la mionzi lililojengwa Kimbiji likiwa limekamilika ambapo utaratibu wa kuweka mashine ili huduma ianze kutolewa unaendelea.*

**PIKIPIKI ZA WATENDAJI WA KATA.**

Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kupitia mapato yake ya ndani ilifanikiwa kununua pikipiki 9 zenye thamani ya Milioni 23.1 kwa Watendaji wa Kata 9 wa Manispaa ikiwa ni uwezeshwaji wa vitendea kazi vitakavyowawezesha kutimiza majukumu yao vyema ikiwa ni pamoja na kuwafikia wananchi pindi wanapowahitaji, kufatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye kata zao na kusimamia ukusanyaji wa mapato.




*Katibu Tawala Dalmia Mikaya akikabidhi namba ya pikipiki kwa Mtendaji wa Kata ya KisaraweII Theophilda Christopher (katikati ) Mstahiki Meya Mhe.Ernest Mafimbo*

# KIGAMBONI 2021

## Miradi kabambe iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani

**UTOAJI WA MIKOPO YA 10%**

Wilaya ya Kigamboni imekua ikitekeleza agizo la Serikali kwa kutenga 10% ya mapato yake ya ndani kwaajili ya kutoa mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi vya wajasiliamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilitenga kiasi cha Mil.434 ikiwa ni makisio ya bajeti ya mapato ya asilimia 10 ambapo hadi kufikia Juni 2021 mapato halisi ya 10% yalikua Milioni.699.

Hadi kufikia Juni 30, 2021 jumla ya Milioni 885.1 zilitolewa kwa vikundi 91 vya wananawake , vijana na watu wenye ulemavu sawa na asilimia 162. Kati ya fedha hizo Milioni 211.6 ni fedha zilizotokana na marejesho yaliyofanywa na vikundi vilivyowahi kunufaika na mikopo na Milioni 673.5 sawa na silimia 96.3 ni fedha zilizotokana na 10% mapato ya ndani.




*Baadhi ya Bajaji zilizotolewa kama Mikopo kwa vikundi vya Vijana.*

Manispaa tangu kuanzishwa kwake mwaka wa fedha wa 2016/2017 hadi 2020/2021 imekwishatoa mikopo yenye thamani ya Bilioni 2.4 kwenye vikundi 551 vyenye jumla ya wanufaika 5095 kati ya vikundi hivyo vikundi vya wanawake 319, vikundi vya vijana 214 na vikundi vya watu wenye ulemavu 18.




*wanakikundi wa kikundi cha Wanawake cha Tushikamane group wakiwa wameshikiria bango la hundi ya mkopo uliotolewa na Manispaa kwenye hafla fupi iliyofanyika ukumbi wa Kibada garden ikiwa ni utekelezaji wa agizo la kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwaajili ya makundi maalumu*

**UJENZI NYUMBA YA MKURUGENZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni katika eneo la utawala bora ilipanga bajeti kwaajili ya ujenzi ya nyumba ya Mkurugenzi kupitia mapato yake ya ndani kiasi cha Milioni.190 ambapo hadi sasa ujenzi umekamilika kwa asilimia 99 sehemu iliyobaki ni marekebisho madogomadogo.

Ujenzi wa Nyumba hii umeweza kusaidia kiongozi kukaa karibu na maeneo yake ya kazi hivyo kuweza kumrahisishia kutoa huduma kwa wananchi kwa wakati na ukaribu zaidi.

**UJENZI WA UZIO SHULE YA SEKONDARI PAUL MAKONDA.**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni pia ilitenga bajeti kiasi cha Milioni 25 kwaajili ya ujenzi wa uzio kwenye shule mpya ya Paul Makonda ili kuimarisha usalama wa wanafunzi na kulinda mipaka ya shule dhidi ya uvamizi.

# Miradi kabambe iliyotekelezwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani

**UJENZI WA MWALO WA SAMAKI BUYUNI**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kupitia mapato yake ya ndani ilifanikiwa kutenga kiasi cha Milioni.200 za kujenga mwalo wa Samaki Kata ya Pembamnazi ili kuchochea na kukuza shughuli za uvuvi na biashara. Hadi sasa mradi upo kwenye hatua za ukamilishwaji na kiasi cha Milioni.167 zilikwisha tumika kufikia Juni na mradi umeanza kutumika.

Kwa kupitia mradi huu wa mwalo wafanyabiashara na wavuvi 567 wameweza kunufaika pamoja na kuwezesha vikundi 84 vya ufugaji mikopo yenye thamani ya Milion 361.2 na vikundi 3 vya uvuvi vyenye thamani ya Milioni 57.8.



*Muonekano wa ndani wa Mwalo wa Samaki uliojengwa Buyuni kata ya Pembamnazi kwa lengo la kuchochea na kukuza shughuli za uvuvi.*

**UJENZI WA ZAHANATI YA MAWENI.**

Ujenzi wa Zahanati ya Maweni ni mradi ulioibuliwa na kutekelezwa na wananchi wa mtaa wa Maweni ili kusogeza karibu huduma za afya ,kwani idadi ya watu ya Mtaa wa Mji mwema imekuwa kubwa kwakuwa na jumla ya wakazi wapatao 14642.

Gharama za mradi ni milioni 50.7 ambapo milioni 27 ni mchango kutoka kwa nguvu za wananchi ambazo zilitumika kujenga jengo kuanzia hatua ya msingi hadi boma.

Manispaa ilifanikiwa kuchangia jumla ya M.23.2 kutoka mapato yake ya ndani ambazo zilitumika katika hatua ya upauaji wa Jengo, kuweka miundombinu ya umeme, majitaka na kupiga plasta ndani nje.

Hadi kukamilika kwa mradi huu Juni 2022 unatarajia kuhudumia wananchi wa Maweni na Mitaa ya karibu hivyo utasaidia kusogeza huduma za afya hususani huduma za mama na mtoto ambapo awali iliwalazimu kutembea umbali mrefu kuzifuata.



*Ujenzi wa Zahanati ya Maweni*

## Mambo 5 msisitizo wa DC Fatma kwa Watendaji wa Kigamboni

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangasa alifanya kikao kazi na wakuu wa Idara na vitengo, Watendaji wa Kata na Mitaa kwa lengo la kufahamiana lakini pia kuwekeana mikakati mizuri katika kuhakikisha lengo la Serikali linafikiwa.

Akizungumza na wataalamu hao kwenye ukumbi wa Manispaa Mhe. Fatma alisema kuwa kwanza angependa kuona ushirikianao unapewa kipaumbele katika kutekeleza majukumu ikiwemo kuona maeneo ya Mapato, Kero za wananchi, ulinzi na usalama, usafi pamoja na usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo (MKUUU) yanapewa kipaumbele.

Akizungumzia suala la ukusanyaji mapato Mhe. Fatma alisema kuwa ni vyema kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato vilivyoainishwa vinakusanywa vizuri, kuongeza bidii ya kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vinaweza kuiongezea Manispaa Mapato, kuhakikisha mianya ya upotevu wa mapato yote inadhibitiwa kwa ukamilifu, ikiwa ni pamoja na kudhibiti fedha za umma kwa kufanyia matumizi kwa kuzingatia taratibu na kanuni.

Kwa upande wa kushughulikia kero aliwaasa Watendaji wa Kata na Mitaa kuepuka kuwa sehemu za migogoro na badala yake kuwa sehemu ya utatuzi kwa kusimamia haki, kuzingatia kufanya mikutano ya kisheria kwa ngazi za chini (Kata na Mitaa) na kuhakikkisha wanatoa taarifa sahihi kwa wananchi.
Aidha aliwataka Watendaji wa Kata na Mitaa kuhakikisha wanaainisha migogoro ya ardhi iliyopo kwenye maeneo yao kwa kuonesha chanzo na namna ambavyo wanapendekeza itatuliwe, kuandalia taarifa na kuipeleka ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Aliongeza kwa kuwataka maafisa utumishi kutatua kero za watumishi kwa kuwafata mahali walipo na kwa kuanzia aliwataka maafisa hao kushughulikia kero zinazowakabili waalimu.

Eneo la ulinzi na usalama Mkuu wa Wilaya alisema Watendaji wa Kata na Mitaa ndio watu muhimu katika kuhakikisha ulinzi na usalama upo katika maeneo yao hivyo ni vyema wakaimarisha vikundi vya ulinzi na usalama vilivyopo kwenye maeneo yao, na kuhakikisha wanasimamia na kudhibiti upitishwaji wa bidhaa za magendo kwenye maeneo yao na uhamiaji haramu.

Katika suala la usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo alisema ni muhimu kuhakikisha wananchi wanashirikishwa katika utekelezaji wa miradi kwa kuwapa uelewa wa kutosha na kuwafanya waone wao kuwa ni sehemu ya miradi iliyopo kwenye maeneo yao.
Watendaji wa Kata na Mitaa walitakiwa pia kuhamasisha wananchi wa Kigamboni kuhusiana na kujilinda kwa kuchukua tahadhari dhidi ya wimbi la tatu la ugonjwa wa korona.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ndg. Erasto Kiwale alisema kuwa ,anaahidi kuhakikisha maelekezo yote yaliyotolewa kufanyiwa kazi kwa weledi na kwamba amefurahishwa na neno la mkuu wa Wilaya kutaka kuwa sehemu ya maendeleo ya Kigamboni na kuhimiza ushirikiano jambo ambalo ni jema katika ufanisi wa kazi .



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa akiwasilisha mambo 5 kwa Watendaji, kushoto ni Mkurugenzi wa Manispaa Erasto Kiwale na Kulia ni Katibu Tawala Dalmia Mikaya*

# Baraza la Madiwani laiomba Wizara ya Ardhi kuliachia eneo la Tungi (Dampo) kuwa Miliki halali ya Kigamboni

Baraza la madiwani kwa Pamoja liliomba wizara ya ardhi kuliachia eneo la tungi (eneo la dampo) ambalo Manispaa lilijipangia matumizi kwa lengo la kuongeza mapato kwa kutumia wawekezaji baada ya jitihada za awali kutoleta matokeo chanya.

Akizungumza kwa niaba ya Madiwani Mstahiki Meya Mhe. Ernest Mafimbo alisema ni takribani miaka miwili wamekuwa wakifuatilia umiliki wa eneo hilo ambalo lipo ndani ya Manispaa ili kuweza kulitumia kwani kwa sasa eneo lile limeonekana kutokuwa na chochote kinachoendelea zaidi ya kulundikwa takataka.

“ Tuliwaelekeza watendaji kurudi tena Wizarani ikiwezekana wamfikie hadi Waziri na kuona namna bora ambayo inaweza kufanyika ili lile eneo liweze kuwa miliki halali kwa Manispaa kwani mpango wa matumizi tulionao ni Mzuri na kwakiasi kikubwa umelenga kuongeza Mapato yatakayotuwezesha kutekeleza miradi yetu ya maendeleo”Alisema Meya

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Erasto Kiwale alizungumzia mafanikio ya Mwaka wa fedha uliopita na mipango ya mwaka wa fedha ujao aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani Pamoja na watendaji kwa ujumla kwa namna ambavyo wameweza kushirikiana kwenye suala la utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususani katika ukusanyaji mapato kwa kufikia 109%.

Aidha pia aliishukuru sana Serikali kuu kwa kuendelea kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Manispaa kwa kuipatia fedha zaidi ya asilimia 94 ambazo zilielekezwa kwenye sekta ya elimu, ambapo kwenye elimu bila malipo Elimu Msingi Mil.400 , Elimu sekondari zaidi ya Bil.1, Sekta ya afya kwa kuongeza ujenzi wa wodi 3 Hospitalini milion 500, milioni 150 kwaajili ya kuendeleza Zahanati na ujenzi wa vituo vya afya 2 vya Tundwi Songani milioni 400 Pamoja na Chekeni Mwasonga milioni 500.

Aliongeza kuwa Sekta ya elimu imekuwa na changamoto kubwa sababu ya ongezeko la wanafunzi kutokana na elimu bila malipo kama ambavyo taarifa ilivyoonesha hivyo wamejipanga kuhakikisha wanaboresha miundombinu kwa kutenga Milioni 800 kutoka mapato ya ndani kwa elimu Msingi na Sekondari ikiwa pia ni utekelezaji agizo la Serikali kupitia TAMISEMI.

Kwa upande wa Miundombinu ya barabara na mitaro alisema imekuwa ni changamoto nyingine kubwa kwani kwa awamu zilizopita Kigamboni haikuweza kuwekwa kwenye miradi ya DMDP na ilibaki nyuma sana sababu ya ule mpango wa KDA ambao haukuruhusu uendelezaji Hivyo, kama Manispaa imeweka bajeti ndogo kwa kuanzia kama Milioni 144 ambazo zitaelekezwa kwenye kusaidia kuboresha miundombinu hiyo na itaendelea kuongeza fedha kadri ya mapato yatakavyokuwa yanaongezeka.

Mkutano wa Baraza wa kufunga mwaka wa fedha 2020/2021 ulifanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Kigamboni.



*Waheshimiwa Madiwani wakifatilia kwa makini mrejesho wa taarifa ya umiliki wa eneo la Tungi kutoka kwa mtaalamu(haonekani pichani)*

# Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Amos Makala awataka wataalamu wa Idara ya Ardhi kutatua kero

Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Amos Makala aliwataka wataalamu wa idara ya Ardhi Manispaa ya Kigamboni kuhakikisha wanatatua kero za wananchi kwa juhudi zote ili kuepuka migogoro.

Mheshimiwa Makala alitoa wito huo mchana katika Mkutano wa kusikiliza kero za wananchi uliofanyika katika uwanja wa Mjmwema ikiwa ni utaratibu aliyouanzisha kwa lengo la kuwafikia wananchi katika majimbo yao.

“Niwahakikishie katika utaratibu huu nitakuwa nanyi kusikiliza hadi hatua ya mwisho nimejitoa kuwatumikia nitakuwa nanyi hadi hatua ya mwisho.” Alisisitiza

Wakati huo huo Mhe. Makalla alizitaka Taasisi zote kubwa zilizoshika maeneo makubwa Kigamboni kujitokeza Mara moja katika Serikali za Mitaa husika na kuyatambua maeneo yao, kuyasafisha na kuyaendeleza ili kuepuka Migogoro na wakazi jirani na maeneo hayo.

Kuhusu changamoto ya Maji, Umeme na Barabara Mhe.Makalla alisema kuwa jumla ya shilingi Billioni 24.7 zimetengwa ili kutekeleza Mradi Mkubwa wa Maji wa visima vya Kimbiji na Mpera ambapo maji hayo yataenda kunufaisha Kata zote za Kigamboni.

Aidha, aliongeza kwa kusema kuwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan



*Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam Mhe. Amos Makalla akizungumza na wananchi wa kigamboni waliofika kutoa kero zao ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kwa Viongozi wa Wilaya ya Kigamboni juu ya utatuzi wa Kero .*

ameshaidhinisha shilingi Billioni 3 ili kutekeleza Mradi Mkubwa wa Tarura pia zaidi ya shilingi Billioni 1.7 zimekwishatengwa ili kuunganisha Umeme katika sehemu zisizokuwa na Umeme.

Naye Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kigamboni Mheshimiwa Ernest Ndamo Mafimbo alimpongeza Mkuu wa Mkoa kwa utaratibu mzuri aliouanzisha kwa kuhamishia shughuli zake Majimboni kwa kusikiliza kero za Wananchi na aliomba utaratibu huo kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mafimbo pia alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kuchanja chanjo ya ugonjwa wa corona ikiwa ni njia sahihi ya kujilinda na ugonjwa huo.

Sambamba na hilo Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mheshimiwa Fatma Almasi Nyangassa alieleza kuwa Wananchi wa Kigamboni walifarijika sana kwa ujio wa Mkuu wa Mkoa na wako tayari kuwasilisha kero zao.





*Pichani ni baadhi ya wananchi waliofika kuwasilisha kero zao kwenye Mkutano wa Kusikiliza kero za Wananchi uliofanyika viwanja vya mjimwema*

## "Asante NMB, tunaomba muendelee kutushika mkono Kigamboni" DC Fatma



*Meneja wa NMB kanda ya Dar Es Salaam Donatus Richard na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa wakizungmza na kusisitiza ushirikiano wakati wa makabidhiano ya madawati ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Ungindoni*

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa aliwashukuru NMB kwa msaada wa vifaa vyenye thamani ya zaidi ya M.25 walivyotoa katika Hospitali ya Wilaya ( mabenchi 50 ya kupumzikia wagonjwa) , Madawati 50 shule ya msingi Ungindoni , mabati 200 Shule ya Msingi Rahaleo na mabati 180 Sekondari ya Kigamboni ikiwa ni sehemu ya kurejesha faida kwa jamii.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo Mkuu wa Wilaya alisema vifaa walivyovitoa vitasaidia kuboresha utoaji huduma na kitendo cha NMB kuichagua Kigamboni kimeonesha ushirikiano mzuri walionao kwani wangeweza kwenda kwingine sababu wahitaji ni wengi.

Aliongeza kwa kusema kuwa changamoto haziishi lakini tunaowajibu wa kuhakikisha tunatatua moja moja kwa kadri nafasi inapopatikana hivyo, hivyo, amewaomba NMB kuendelea kuishika mkono. Kigamboni katika kusaidia juhudi za Serikali za kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Wakati huohuo aliwataka wahudumu wa Afya na Walimu wa Shule waliopokea vifaa kuhakikisha wanavitunza na kutumia kadri ya mahitaji ili kuwapa morali NMB na wadau wengine kuendelea kuiona Kigamboni inastahili kupewa kipaumbele katika kuunga mkono juhudi za maendeleo.

Mstahiki Meya wa Manispaa Mhe. Ernest Mafimbo aliwashukuru NMB kwa niaba ya wananchi na kusema kuwa Serikali haina uwezo wa kutatua changamoto zote kulingana na ufinyu wa bajeti hivyo wanapotokea wadau kama NMB inakuwa inaisaidia katika utoaji huduma bora.

Meneja wa NMB kanda ya Dar es Salaam Donatus Richard aliishukuru kigamboni kwa ushirikiano na kuwatambua kama wadau wa maendeleo na kusema kuwa itaendelea kutoa ushirikiano kwani kila mwaka imekua ikitenga 1% kwaajili ya kurudisha faida kwa jamii na wamelenga maeneo ya Afya, Elimu na Majanga yasiyotegemewa.

Aliongeza kusema kuwa kwa mwaka uliopita walitenga zaidi ya Tsh. Bilioni 2 ili itumike katika kurejesha kwa jamii , wao Kigamboni ni jamii yao na wamekuja kuadhimisha rejesho kwa jamii kwani hawawezi kuendelea kama jamii haipo.



*Meneja wa NMB kanda ya Dar Es Salaam Donatus Richard akifurahi na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa wakati wakikabidhiana Mabati eneo la Shule ya Msingi Ungindoni.*

# KIGAMBONI 2021

## Baraza la Madiwani lapitisha Taarifa ya hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa mikono miwili



*Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kigamboni Mhe. Ernest Mafimbo katikati akihitimisha upokeaji wa taarifa za Hesabu, kushoto ni kaimu Mkurugenzi Charles Lawiso na kulia ni Naibu Meya Mhe. Stephano Wryoba.*

Baraza la Madiwani Manispaa ya Kigamboni kwa pamoja lilipitisha taarifa ya hesabu za mwisho yaani Final Accounts zilizoishia 30.06.2021 ikiwa ni takwa la kisheria na kuwapongeza watendaji kwa kukamilisha taarifa hiyo ikiwa ni mwaka wa tano kwa Halmashauri kufunga hesabu zake tangu kuanzishwa na kupata hati safi kwa miaka minne mfululizo.

Akiwasilisha taarifa hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Idara ya Fedha Jenoveva Meshi alisema kwa mwaka huu wa fedha 202/2021 imefunga vitabu vitano vya hesabu za mwisho ambavyo ni, Kitabu kikuu (consolidated financial statements), Mfuko wa afya ya pamoja (Health Basket financial statements 202/2021), ment).
Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye wenye ulemavu (women,youth and disability financial statement), mradi wa tofali (Bricks projects financial statement), na Mfuko wa kunusuru Kaya Masikini (TASAF project financial statement).

Aidha katika kikao hicho Diwani wa Kata ya Kigamboni Mhe.Dotto Msawa alishauri kuepuka baki ya fedha kwa fedha zinazoletwa na serikali kuu kwajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa Charles Lawisso alisema kuwa amepokea mapendekezo yote yaliyotolewa ikiwa na kujitahidi kutumia fedha kadri zinavyoletwa ingawa wakati mwingine inakua ngumu kutokana na sheria za manunuzi kubana na fedha hizo kutofika kwa wakati.

Taarifa za uwasilishwaji wa hesabu za mwisho zilifanyika kwenye kikao cha Baraza maalumu lililofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa.



*Mhasibu Jenoveva Meshi akiwasilisha taarifa ya ufungaji wa Hesabu kwa niaba ya Mkuu wa Idara ya Fedha*

## Jamii yaaswa kuenzi misaada ya wadau

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe Fatma Almasi Nyangasa aliwataka walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla kuenzi na kutunza Samani mbalimbali zinazotolewa na wadau ikiwa ni njia ya kuheshimu michango hiyo katika secta mbalimbali.

Mhe Nyangasa alitoa wito huo alipokuwa akipokea msaada wa viti pamoja na meza zake 200 vilivyotolewa na shirika la Bima (NIC) vyenye thamani ya shilingi Mil 20 Katika hafla fupi iliyofanyika shule ya Sekondari Aboud Jumbe iliyopo Manispaa ya Kigamboni.

Katika makabidhiano hayo Mhe Mkuu wa wilaya pia alisema Serikali inatambua mchango wa vijana katika kukuza maendeleo ya nchi kupitia nyadhifa ya chini kwa kutatua changamoto katika sekta ya

# KIGAMBONI 2021

## Jamii yaaswa kuenzi misaada ya wadau

elimu.

Akitoa msaada huo mwakilishi wa Meneja wa shirika la Bima Ndugu Karimu meshack ambaye ni Meneja Uhusiano katika shirika hilo alisema, Shirika limetoa msaada huo ikiwa ni kutambua juhudi za Serikali katika kuboresha secta ya elimu kupitia sera ya elimu bila malipo ambapo uhitaji wa viti na meza umekuwa ni changamoto kubwa kutokana na muitikio mkubwa wa jamii.

Aidha Meneja Uhusiano aliahidi kuendelea kushirikiana na Wilaya ya Kigamboni katika kutatua changamoto mbalimbali hususani katika sekta ya elimu.

Akiongea kwa niaba ya Wanafunzi wa Aboud Jumbe mwanafunzi Lusajo Mwasilu alipongeza Shirika kwa kuwapatia nyenzo zitakazowasaidia katika masomo yao na kuahidi kufanya vizuri katika masomo yao kupitia msaada huo.

Shirika la Bima lilitoa jumla ya viti na meza 200 vilivyogawanywa katika shule 3 ambazo ni shule ya Sekondari Aboud Jumbe viti na meza 100, Kisarawe II viti na meza 50, pamoja na Minazini Viti na meza 50




*Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Aboud Jumbe wakiwa wameketi kwenye viti na meza zilizotolewa na Shirika la NIC kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia wanafunzi*

## Maafisa Ugani Kigamboni wajengewa uwezo mafunzo ya M-Kilimo



*Maafisa Ugani wa Kigamboni wakigatilia kwa makini mafunzo ya mfumo wa M-Kilimo*

Maafisa ugani wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni walipatiwa mafunzo ya namna ya kutumia mfumo wa M-Kilimo kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waweze kuhudumia wakulima kwa weledi na ukaribu.

Mkufunzi wa mfumo huo Mhandisi wa Kilimo Rajab Kitilige alisema wameamua kutoa mafunzo ya ana kwa ana kwa wagani ili kuboresha utoaji huduma kwani awali walifanikiwa kufanya mafunzo kwa njia ya mtandao pekee

Aliongeza kwa kusema kuwa Mfumo wa M-Kilimo umegawanyika katika maeneo mawili ya kutoa huduma ya ushauri kwa wakulima juu ya huduma za ugani na kuunganisha wakulima na wanunuzi wa mazao yao.

Mafunzo hayo yalifanyika kwenye ukumbi wa Manispaa na yalitolewa na Mkufunzi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, mhandisi wa Kilimo Bw. Rajabu Kitigile.

# Halmashauri ya CCM Wilaya ya Kigamboni yaipongeza Manispaa kwa ukusanyaji mzuri wa mapato.

Halmashauri ya chama cha mapinduzi CCM Wilaya ya Kigamboni ikiongozwa na mwenyekiti wake wa Wilaya Henry Chaula kwa pamoja waliazimia kutoa tamko la kuipongeza Manispaa na Wilaya ya Kigamboni kwa ujumla kwa kufanya vizuri kwenye zoezi la ukusanyaji mapato kwa kuvuka lengo la mwaka walilokuwa wamejiwekea kutoka Bilioni 7.7 hadi Bilioni 8.1 sawa na asilimia 105.4 kwa kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Juni 20, 2021.

Pongezi hizo zilitolewa wakati walipokuwa wakipokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwaajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2021 ambapo alisema kuwa Kigamboni ya sasa si ile ya kwanza kwani mabadiliko yanaonekana na kwamba hiyo ni kazi nzuri ya watendaji.

Aidha Mwenyekiti Henry aliwaelekeza Watendaji kutumia nguvu kubwa katika kutoa elimu kwa wananchi na kutumia lugha nzuri katika kila eneo wanalojihusisha na wananchi badala ya kutumia nguvu .

Katika kuhakikisha Kigamboni inazidi kukua na kusonga mbele kimaendeleo Mwenyekiti Henry aliwataka Watendaji kufanya kazi kwa uadilifu ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi maboresho yaliyotolewa na wajumbe mbalimbali pindi walipokuwa wakijadili taarifa ya utekelezaji.



*Mwenyekiti wa CCM Wilaya Henry Chaula akipongeza Wilaya na Manispaa kwa kukusanya vizuri mapato kwa niaba ya wajumbe wote.*

Halmashauriya CCM pia iliwapongeza TRA Kanda ya Kigamboni kwa ukusanyaji mzuri wa mapato ambapo kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2021 ililenga kukusanya 2.2 Bilioni na kufanikiwa kukusanya Bilioni 2.5 hadi kufikia Juni 10, 2021.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa aliishukuru Halmashauri ya wilaya CCM kwa maoni mbalimbali na maelekezo waliyoyatoa kwa lengo la kuiboresha Kigamboni na kuahidi kuhakikisha yanafanyiwa kazi kwa uaminifu.

Kikao hicho kilifanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ambapo Taasisi za TARURA, DAWASA,TANESCO,TRA na Wakala wa Vivuko TEMESA walishiriki katika kutolea ufafanuzi hoja mbalimbali na kupokea ushauri uliotolewa.



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Erasto Kiwale akiwasilisha taarifa kwenye kikao cha kupokea taarifa ya Utekelezaji wa Ilani.*

# KIGAMBONI 2021

## LEAT na Manispaa ya Kigamboni Ushirikiano wenye matumaini katika mapinduzi ya kimazingira.

Diwani wa Kata ya Tungi na Mstahiki Meya wa Manispaa ya kigamboni Mhe. Ernest Mafimbo alisema kuwa anaimani ushirikiano wa LEAT katika mapinduzi ya kimazingira utakua na matokeo chanya na kuacha alama hata baada ya kumaliza muda wake.

Mstahiki Meya aliyasema hayo kwenye ofisi ya Mtaa wa Magogoni alipokuwa na wataalamu wa LEAT waliofika kupata muongozo wa kutembelea maeneo yenye changamoto ya kimazingira ili kufahamu jitihada zilizofanywa na Manispaa na wao kama Tasisi kuona namna wanaweza kutoa msaada.

Akitolea ufafanuzi Meya alisema kuwa Kata ya Tungi inachangamoto kubwa lakini kwa kutumia wadau mbalimbali ikiwemo wajumbe wa nyumba kumi na mabalozi wameendelea kuchukua jitidaha za kupambana na uharibifu wa kimazingira ikiwemo kuweka ulinzi na kutoa elimu ambayo bado inaendelea kutolewa ili kuwafanya wananchi kutambua umuhimu wa kutunza mazingira kwa mstakabali wa Afya na maendeleo kwa ujumla.

Kwa upande wake afisa mazingira wa Manispaa Bw. Sixbert Kyaruzi alisema kuwa kumekuwa na tabia ya wananchi kuvamia viwanja visivyoendelezwa na kutupa taka, kama wataalamu wamekuwa wakifanya juhudi za kuwatambua wamiliki na kuwapa notisi za kuendeleza



*moja ya eneo la Mtaa wa Magogoni lililoathirika na ujenzi holela uliopeleka kuziba mkondo wa maji hatimaye kusababisha maji kutuama nyakati zote za kiangazi na masika.*

maeneo yao ili kudhibiti hali hiyo.

Kyaruzi alisema kuwa anaamini mbali na kusimamia sheria , tatizo la utupaji taka kwenye maeneo yasiyo rasmi litadhibitiwa pindi mradi waujenzi wa dampo la kisasa Kisarawe II utakapokamilika.

Afisa Mazingira wa LEAT Agnes Ng'wandu alisema Taasisi yao itaendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuandaa semina kwa viongozi wa ngazi za Manispaa, Kata na Mitaa ili kusaidiana katika jitihada za kudhibiti suala la uharibifu wa mazingira.

LEAT ni Taasisi isiyo ya Kiserikali inayoshughulika na masuala ya ulinzi na uhifadhi mazingira na rasilimali za maliasili inayofanya kazi kwa kushirikiana na Manispaa za Mkoa wote wa Dar es Salaam ambapo kwa Kigamboni wamekwisha kutembelea Kata za Vijibweni, Kigamboni, Tungi na Kibada.



*Wataalam wa LEAT na Viongozi wa Manispaa walipotembelea eneo la Vijibweni*



*wataalamu wa LEAT na viongozi wa Manispaa walipotemnelea eneo la Feri kuona uharibifu mazingira*

# KIGAMBONI 2021

## Miradi yenye thamani ya Bilioni 1.3 ilipitiwa na Mwenge maalumu wa Uhuru mwaka 2021

Mwenge wa Uhuru 2021 Wilayani Kigamboni ulikimbizwa kilometa 82.3 katika Tarafa tatu (3) (Kigamboni, Somangila na Pembamnazi) na Kata tano (5) (Vijibweni, Kigamboni, Mjimwema, Somangila na Kimbiji).

Mwenge huo uliweza kupitia miradi ya maendeleo ya ujenzi mitano (5) katika Sekta za Afya miradi miwili (Uwekaji mawe ya msingi katika miradi ya ujenzi wa Zahanati na Jengo la Mionzi katika Kituo cha afya Kimbiji), Elimu miradi miwili (Uzinduzi wa Jengo la Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Elimu na Uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa Bweni la Wanawake shule ya Sekondari Kimbiji) na Barabara mradi mmoja (Ujenzi wa Barabara ya Azimio – Mashujaa yenyeurefu wa kilomita 1,46) na kukagua shughuli za mradi wa kikundi cha VEMA na mradi mmoja (1) uliopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru za mwaka 2019 (Ukarabati wa Kisima cha Maji Gezaulole) .

Miradi hiyo iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 ilikuwa na thamani ya Sh. 1,306,469,431.75 zikiwemo Sh. 31,110,000.00 za michango na nguvu za wananchi, Sh. 113,226,829.64 za Mapato ya Ndani ya Halmashauri na Sh. 1,162,132,602.11 fedha toka Serikali Kuu.

Aidha kwenye uwanja wa mkesha Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 ulikagua mabanda mbalimbali ya shughuli za Kiuchumi na Kijamii ikiwemo mabanda ya mapambano dhidi ya dawa za Kulevya, mapambano dhidi ya Malaria, TAKUKURU, Vikundi vya Kiuchumi, Mfuko wa Afya ya Jamii, masuala ya Lishe, mapambano dhidi ya VVU/ UKIMWI, TEHAMA, Watu wenye Ulemavu na Maonyesho ya shughuli za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

## HABARI KATIKA PICHA



*Wataalamu wa Manispaa na Wilaya wakifatilia taarifa ya utekelezaji wa Ilani kwenye ukumbi wa Manispaa*



*Wajumbe wa Kamati ya CCM Wilaya na wataalamu wa Manispaa wakiwa kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo*



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni akishika mwenge wa Uhuru ishara ya ukakamavu eneo la Mkesha.*



*Ziara ya Madiwani na Wataalamu kuona maeneo ya uwekezaji Urithi kutoka Manispaa ya Temeke.*



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**
**S.L.P 36009, DAR ES SALAAM**
**www.kigambonimc.go.tz**